TANGAZO LA SERIKALI Na. 804 la tarehe. 13/9/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA

SURA YA 147

# AMRI

*(lmetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA AJILI YA MIRADI YA MAJI KATIKA MIJI YA KIOMBOI, SINGIDA, MANYONI, CHAMWINO, CHEMBA NA MUGUMU KWA KAMPUNI YA MEGHA ENGINEERING AND INFRASTRUCTURES LTD, YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Miradi ya Maji Katika Miji ya Kiomboi, Singida, Manyoni, Chamwino, Chemba na Mugumu kwa Kampuni ya Megha Engineering and Infrastructures ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kama meanza kutumika tarehe 11 Disemba 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayowezakuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa Saruji iliyoanishwa katika Jedwali la Amri hii, iliyoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Kampuni ya Megha Engineering and Infrastructures kwa ajili ya Miradi ya Maji katika Miji ya Kiomboi, Singida, Manyoni, Chamwino, Chemba na Mugumu unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa saruji itatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yaliyotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 10 Disemba 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| No | Maelezo | Kipimo | Kiasi |
|---|---|---|---|
| 1 | Saruji | Kilogram | 15,000,000 |

Dodoma,
3 Septemba, 2024

MWIGULU LAMECK CHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*